# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UTALII BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA 2026/2027

------------------

**Mheshimiwa Spika**, kwa ruhsa yako, naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za Kawaida na Maendeleo kwa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa Mwaka 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaaliwa uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana kwa mara nyengine tena katika chombo hiki muhimu kwa ajili ya ustawi wa wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza letu hili, kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa uweledi na umahiri mkubwa, namuaomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima na busara ili tuweze kufikia malengo na wajibu wetu katika chombo hiki adhimu na muhimu kwa nchi yetu.

Vile vile, tunatoa pongezi kwa Uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa ushirikiano wanaotuonesha katika utekelezaji wa kazi zetu, Kamati inawaomba waongeze ushirikiano huo pamoja na bidii na ari katika kutekeleza na kusimamia majukumu yao kwa ubora na ufanisi zaidi ili kufikia malengo yalilokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upekee kabisa nawashukuru Wajumbe wezangu wa wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kutoa katika kutekeleza kazi za Kamati hii na hatimae tukaweza kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza letu Tukufu, kama maelekezo ya Kanuni ya 103 (6) ya Kanuni zetu za kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2024 kuhusiana na uwasilishaji wa maoni ya Kamati yanayohusu Makadirio ya kila Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba sasa kuwatambua Wajumbe walioshiriki hadi kukamiliki ripoti hii kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Dkt Mohamed Ali Suleiman | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abdulghani Ismail Zubeir | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Said Ali Juma | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Moza Mohamed Khamis | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Juma Usonge Juma | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Said Azana Hassan | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |
| *9.* | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |
| *10.* | Ndg. Hafidh Ussi Haji | Afisa wa Bajeti |

## UKUSANYAJI WA MAPATO

**Mheshimiwa Spika,** tunaanza kutoa maoni ya Kamati yetu kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa kuangalia mapato ya Wizara yanayokwenda Hazina, ambapo kwa mwaka huu wa fedha 2026/2027, Wizara imekadiriwa kukusanya **TZS Bilioni 2.25** ambapo katika kipindi cha upimaji cha miezi Tisa, Wizara haikufikia lengo na badala yake imekusanya **TZS Bilioni 1.272** sawa na asilimia **57%** tu za makadirio.

**Mheshimiwa Spika,** Uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba, hatua hii ni kurudi nyuma ukilinganisha na asilimia **96.3%** ya ukusanyaji mwaka 2025/2026 katika kipindi kama hiki cha upimaji. Kamati inawaomba watendaji wa Wizara hii kuongeza bidii ya utendaji utakaopelekea kukusanya zaidi na hatimae kufikia malengo ya makadirio yaliyopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Kamisheni ya Utalii inaonekana kujipanga vizuri zaidi na kufanikiwa kukusanya hadi asilimia **90%** za makadirio. Kwa kweli, hatua hii ni ya kutia moyo na yakupongezwa kwani inaonesha tofauti kubwa ya mafaniko kulinganisha na ukusanyaji wa asilimia **51%** ya makadirio kwa mwaka 2025/2026 katika kipindi kama hicho cha upimaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaiomba Mamlaka ya Hifadhi ya Uendelezaji Mji Mkongwe kuongeza bidii ya utendaji na ufuatiliaji ili hatimae kukusanya vizuri na kufikia lengo lililokusudiwa. Kamati inatoa wito huu baada ya kuchunguza makusanyo ya Mamlaka hii ambapo katika kipindi cha upimaji cha Miezi Tisa, Mamlaka imekusanya **TZS Bilioni 2.287** sawa na asilimia **63.5.**

## MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa dhati kabisa tunaipongeza Serikali kwa kuhakikisha inaendelea kuweka mazingira bora ya uwekezaji pamoja na kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi na hatimae tukaweza kufikia hatua ya kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini, kutoka watalii 736,755 mwaka 2024 hadi 917,167 mwaka 2025, pamoja na kuongezeka kwa siku za ukaazi kwa mtalii. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuzidi kuboresha huduma za kijamii na kiuwekezaji ili kuhakikisha wataalii hao wanatumia zaidi wanapokua nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu pia inasononeshwa na changamoto zinazoendelea kuripotiwa na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, ikiwemo uvamizi katika maeneo ya Kihistoria pamoja na Uvamizi wa Biashara zinazotakiwa kufanywa na wazawa, na badala yake kuchukuliwa na wageni kinyume na Sheria ya Utalii. Kamati inaishauri Wizara kuongeza kasi na bidii katika kuyahami maeneo hayo kwa kuyapima na kuyahifadhi maeneo ya Kihistoria ili kuondosha uvamizi huo. Aidha, Kamati inahimiza kufuatwa kikamilifu kwa Sheria ya Utalii na kuhakikisha kwamba wageni hawakiuki sheria katika biashara hii ya Utalii.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE.

### Mradi wa Kuimarisha Eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa uwamuzi wa kuyaendeleza maeneo ya kihistoria ikiwemo, eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu Pemba. Kamati ilitembelea eneo hili na kushuhudia hatua kubwa iliyofikiwa katika uimarishwaji wa eneo hili ikiwa ni asilimia 95% ingawa fedha alizolipwa Mkandarasi ilikua ni asilimia 57% tu.
Aidha, uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba, Mradi unakabiliwa na baadhi ya changamoto ikiwemo kutokamilika kwa wakati uliopangwa, jambo ambalo limepelekea kuzorota kwa shughuli za Utalii katika eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu, changamoto ambayo tumebaini imechangiwa na kutopatikana kwa wakati malipo ya awamu ya kwanza, na kuchelewa kupatikana kwa kibali cha ujenzi kutoka *DCU* (*Development Control Unit*).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuendelea kuyafanyia matengenezo maeneo ya kihistoria ili kuleta haiba nzuri na ya kuvutia wageni wanaotembelea maeneo hayo, kwa lengo la kuongeza makusanyo na mapato ya Wizara.

### Eneo la kihistoria la Mwangapwani

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo imeridhika na maendeleo ya Mradi wa Kuimarisha eneo la Kihistoria la Mangapwani hadi kufikia asilimia 95. Hii inatokana na mtiririko mzuri wa upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu ambapo hadi kufikia Mwezi Machi 2026

zilifikia asilimia 87. Kamati inaamini mradi huu utakamilika muda mfupi ujao na serikali nayo itakamilisha fedha zote zilizotengwa ambazo ni **TZS Bilioni 2.238 .**

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla wake, Kamati haikuridhika na uingizwaji wa fedha katika Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe, ambapo kwa mwaka 2025/2026 Programu ilipangiwa kutumia **TZS Bilioni 34.158** na hadi kufikia Mwezi Machi 2026 iliingiziwa **TZS Bilioni 14.946** sawa na asilimia 43.46. Kamati inaendelea kuiihimiza Serikali kuingiza fedha zote kama zililivyoidhinishwa na Baraza lako tukufu, kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa Programu hii.

## PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

**Mheshimiwa Spika,** Katika Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii ambayo inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Utalii, Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo haikuridhika na mtiririko wa upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini. Kamati imebaini kuwa hadi kufikia Machi 2026 programu hii imeingiziwa asilimia **4.75%** tu ya fedha zilizoidhinishwa.

Kamati inaamini kwamba, utalii ni chanzo kikubwa cha ukuaji wa sekta za uchumi, upatikanaji wa ajira na uimarishaji wa maisha yetu. Hivyo, tunaiomba serikali kuiingizia fedha zote kwa ajili ya Programi hii, ili kuiwezesha Idra ya Maendeleo ya Utalii kutekeleza vyema mipango na sera za Utalii, kukuza maendeleo ya Utalii endelevu wa ndani na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile tunasikitika kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, Programu hii iliidhinishiwa **TZS Bilioni 6,** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, lakini hadi kufikia Machi 2026, haijafanikiwa kupata fedha yeyote ya miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imebaini kwamba kukosekana kwa fedha hizo kumepelekea kutoendelezwa miradi iliyopangwa katika maeneo yaliyoibuliwa vivutio vipya vya utalii ikiwemo kijiji cha Muungoni na Uzi kwa Unguja. Eneo la Pango Samaki, Kisiwa Ndege na Mto furaha kwa upande wa Pemba. Hivyo, Kamati inamuomba Mheshimiwa Waziri kulieleza Baraza lako Tukufu hali ilivyo kwa sasa ili kujiridhisha na fedha wanazotaka kiudhinisha kwa mwaha huu wa fedha wa 2026/2027.

## PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kwa dhati kabisa imeridhika na upatikanaji wa fedha katika Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii kwani katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii iliidhinishiwa jumla ya **TZS Bilioni 1.263** kwa kazi za kawaida, na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **TZS Bilioni 1.731** sawa na **asilimia 137.** Kamati inaamini kwamba upatikanaji wa fedha kumeiwezesha Wizara kupitia Kamisheni ya Utalii kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi, kwa kushiriki maonesho ya utalii ya kitaifa , kikanda na kimataifa na hatimae kupata watalii wengi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kumaliza uchambuzi wa Kamati kuhusiana na bajeti ya hii, sasa napenda kukushukuru tena wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuanza kuchangia hoja hii iliyopo mezani. Aidha, napenda kutoa

shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati tunachambua Fungu la Wizara pamoja na wakati wote Kamati inapofanya kazi na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuifuatilia kwa ukaribu sana hotuba yangu hii na kwa kunisikiliza. Ni matumaini yangu kuwa Wajumbe wataichangia, wataijadili na hatimae kuipitisha Bajeti ya Wizara hii kwani imebeba sekta muhimu sana ya nchi yetu ambayo ndio mategemeo makubwa ya kuinua uchumi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono Hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante,



………………………………….

**(Mhe: Dkt. Mohammed Ali Suleiman).**
**Makamu Mwenyekiti,**
**Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**<u>Zanzibar.</u>**